

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO (LGDG) NA MAPENDEKEZO YA MIRADI INAYOTAKIWA
KUANZA KUTEKELEZWA ILIYOWASILISHWA KWENYE CMT TAREHE 9/3/2017 & FUM 14/3/2017**

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2017 Halmashauri imepokea Jumla ya Sh. **81, 833,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za Maendeleo kutoka mfuko wa LGDG. Aidha kulingana na mwongozo mpya wa matumizi ya fedha toka fungu hili ni sharti 10% itengwe kwa ajili ya shughuli za CBG na 10% nyingine kwa ajili ya ufuatiliaji miradi (M&E). Hivyo kwa kuwa fedha za CBG na MEG hazikutengwa kwenye mapokezi ya awali (Desemba 2016) zinatakiwa kutengwa zote kwa pamoja toka fungu hili liliopokelewa Januari 2017. Hivyo Mchanganuo wa mgawanyo wa fedha hizi utakuwa kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali 1:Mapokezi ya Fedha za LGDG

NO	PROGRAMU/MRADI	KIASI KILICHOPOKELEWA
1	Fedha za LGDG zilizopokelewa Desemba 2016	82,060,000
2	Fedha LGDG zilizopokelewa January 2017	81,833,000
	JUMLA KUU YA MAPOKEZI	163,893,000
	10% CBG	16,389,300
	10% MEG	16,389,300
	Jumla CBG & MEG	32,778,600

Kwa vile fedha zilizopokelewa mwezi **Desemba 2016** zote zilipelekwa kwenye fungu la miradi, **CBG** na **MEG** zitatolewa toka fedha zilizopokelewa mwezi **Januari 2017** ambapo fedha zitakazogawanya kweye miradi zitakuwa ni shilingi **49,054,000 (i.e; 81,833,000 - 32,778,600 = 49,054,000)**

Jedwali 2: Miradi inayopendekezwa kupatiwa fedha

	PROGRAMU/MRADI	FEDHA
1	Kukamilisha ujenzi wa Bwalo la Chakula S/Sekondari Mgola (Kata ya Lugenge)	14,980,000
2	Ujenzi wa Bweni la wasichana S/Sekondari Anne Makinda(Kata ya Ihanga)	20,974,000
3	Kujenga banda la kukusanya majani ya Chai -Luponde(kata ya Luponde)	10,000,000
4	Pikipiki moja (Mifugo - 2,500,000) + (600,000 -Nyongeza Kilimo)	3,100,000
	Jumla Miradi	49,054,000
1	CBG na MEG (20%)	32,778,600
	JUMLA KUU (Mapokezi ya Januari 2017)	81,833,000

NB: *Halmashauri inapanga shule ya Sekondari Anna Makinda kuwa ya Kidato cha TANO na SITA kwa wasichana katika Halmashauri ya Mji Njombe hivyo ni lazima miundombinu ya shule hiyo iboreshwé kukidhi mahitaji na hadhi hiyo. Hivyo baadhi ya miundombinu italazimika kutekelezwa toka ngazi ya Halmashauri (Higher Level) na Sehemu kuchangiwa na wananchi (Lower level) ili kuifanya ikamilike kwa haraka*

Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathimini zitazingatia maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango ambayo yanazitaka Halmashauri kufanya mapitio ya bajeti ili kutenga 10% kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi na 10% kwa ajili ya Kujenga uwezo (Capacity Building). Asilimia 10 kwa ajili ya kujenga uwezo zitaanza kutengwa baada ya kufanya mapitio (Re-allocation)

Naomba kuwasilisha

**JUMANNE A. MWANKOO
KNY MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**